

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

JUNI 2016

Muda: Saa 2½

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2½

MAAGIZO

- *Jibu maswali manne pekee.*
- *Swali la kwanza ni la lazima.*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Ushairi, Tamthilia na Fasihi Simulizi.*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

1. USHAIRI

Soma mashairi yafuatayo kasha ujibu maswali.

SIKUJUA!

1. Kama ningefuga ng'ombe, mafahali na vindama,
Zisingenidhuru pembe, ngeu kuniandama,
Samli ni lembelembé, na minofu ya minyama.
2. Kama ningefuga mbuzi, na kondoo kundi zima,
Ningewajengea zizi, na maziwa nikakama,
Ningewachuna na ngozi, kutengenezea ngoma.
3. Kama ningefuga bata, nao kuku kwa ujima,
Chakula siyo matata, ni machicha na mtama,
Mayai ningeyapata, na kitoweo kizima.
4. Kumbe nimefuga punda, mashuzi ndio heshima,
Ni ukaidi na inda, mateke kurusha nyuma,
Nyama limekuwa nunda, mfugaji humuumaa.

Kiitikio

Sikujua wa kufuga, mnyama mwenye faida

SHAIRI B

Afrika na Watu Wake

Mimi ninaona mgonjwa
Bado amelala kitandani.
Kama hatutamtoa miiba iliyobaki
Mgonjwa hataweka miguu yake chini
Ili kutembea bila ya kufiegemeza.

Miiba iliyomo ndani mwetu lazima
Pia iondoewe upesi kabla haijaingia
Kati ya mfupa na kufa pamoja nasi.
Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma
Halafu tucheze nao mchezo wa siasa na uchumi.

Lakini kuitoa miiba hii
Tunahitaji macho makali
Mikono isiyotetemeka
Moyo usio na huruma
Na kuona miiba ilipoingilia.

MASWALI

- (a) Onyesha jinsi ujumbe unaopatikana katika ubeti wa nne wa Shairi A na Shairi la B unavyokatisha tamaa. (Alama 4)
- (b) Eleza maana ya mshororo huu kama unavyojitokeza kwenye ubeti wa pili wa shairi B. (Alama 2)
Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma.
- (c) Linganua sifa za kimundo ukizingatia ubeti wa pili wa Shairi A na Shairi B. (alama 4)
- (d) Ukizingatia Mshororo wa kwanza kwenye ubeti wa pili wa Shairi A, onyesha jinsi Mshairi alivyotumia kibali chake. (alama 2)
- (e) Onyesha sifa moja ambayo inadhihirika kwenye shairi la B na ambayo hutawala tungo za aina hii. (alama 2)
- (f) Nafsi nenii amedhihirisha toni gani kwenye shairi A? (alama 1)
- (g) Taja nafsi mbili nenwa kwenye shairi la B. (alama 2)
- (h) Andika ubeti wa mwisho wa shairi B kwa lugha ya nadhari. (alama 3)

2. KIDAGAA KIMEMWOZEA

1. ‘Wanyonge ndio wanyongwao ni kauli inayodhihirika vyema kupitia wahusika tofauti katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. Jadili. (alama 20).
2. “Alipofikishwa kwenye zahanati hakushughulikiwa ipasavyo.Ubwete ni ugonjwa mmoja mbaya walioambukizwa madaktari na wauguzi wengi Tomoko”
a) Eleza Muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Dhihirisha jinsi mtunzi alivyoitumia tamathali yoyote moja inayobainika kifunguni.(alama 4)
- c) Riwaya Ya Kidagaa Kimemwozea ni muhtasari wa maradhi yanayolihujumu Bara Afrika.Tetea rai hii kwa mifano faafu riwayani. (alama12)

3. FASIHI SIMULIZI

- (a) Eleza dhima ya lakabu kwa kurejelea hoja tano. (alama5)
- (b) Jadili sifa tano za michezo ya watoto. (alama 5)
- (c) Fafanua mambo matano yanayomfanya mtu awe mlumbi bora. (alama 10)

4. MSTAHIKI MEYA

1. Jadili mbinu zifuatazo kama zilivyotumika katika Mstahiki Meya. (alama 20)
- (a) Jazanda
(b) Uzungumzi nafsia
(c) Majazi
(d) Methali
2. Nonsense! Hivi huyu ana nia gani?
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- (b) Taja na ueleze mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
- (c) Jadili umuhimu wa msemaji katika tamthilia hii. (alama 6)
- (d) Jadili njia za kuondoa uozo katika jamii ukijikita katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 6)

5. DAMU NYEUSI

“Ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani”.

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Fafanua sifa zozote nne za mrejelewa (alama 8)
- (c) Eleza fani uliotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (alama 2)
- (d) Kwa kurejea hadithi zozote tatu, eleza namna wahusika wowote watatu walivyoathiriwa na kiu. (alama 6)